# JARIBIO LA MTIHANI

# DARASA LA SITA - MWAKA 2020

# KISWAHILI: LUGHA

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

**1.** Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.

**2.** Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

---

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Mzee Mokaya ____**1**___ akipika wakati wa ____**2**___ mkuu. Alipokuwa akila ____**3**___ mtu angebisha hodi, yeye kwanza alificha chakula mvunguni____**4**_______ kitanda kabla____**5**___ kujibu karibu. Mgeni alipoingia alikaribishwa____**6**___ na wakaongea____**7**___ muda ____**8**___ kutosha. Mara tu mgeni____**9**___ mzee alitoa chakula chake na kuendelea____**10**___.

Siku ____**11**___ Mokaya alipika wali na kitoweo ____**12**___ kuku wakati wa chakula cha mchana. ____**13**___ chakula na kukiweka ____**14**___. Haya yalidhihirisha dhahiri____**15**___ kuwa Mokaya alikuwa mkono birika.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** ulikuwa | **B.** hakuwa | **C.**alikuwa | **D.**alikua |
| **2.** | **A.**siku | **B.**usiku | **C.** masiku | **D.**cha usiku |
| **3.** | **A.**halafu | **B.**baada | **C.**harafu | **D.**alafu |
| **4.** | **A.**cha | **B.**ndani | **C.**kwa | **D.**mwa |
| **5.** | **A.**ya | **B.**na | **C.**kwa | **D.**yake |
| **6.** | **A.**mzuri | **B.**visuri | **C.**vizuri | **D.**baadaye |
| **7.** | **A.**kwa | **B.**na | **C.**kuwa | **D.**kua |
| **8.** | **A.**ya | **B.**cha | **C.**wa | **D.** mwa |
| **9.** | **A.**atakapoondoka | **B.**aondokapo | **C.**anapoondoka | **D.**alipoondoka |
| **10.** | **A.**kuila | **B.**kukila | **C.**kunywa | **D.**kukula |
| **11.** | **A.**moja | **B.**mmoja | **C.**monja | **D.**mumoja |
| **12.** | **A.**ya | **B.**za | **C.**cha | **D.**la |
| **13.** | **A.**Alikula | **B.**Alipakua | **C.**Alipakia | **D.**Alipagawa |
| **14.** | **A.**mezani | **B.**meza | **C.**kwa meza | **D.**sahani |
| **15.** | **A.**tayari | **B.** shahiri | **C.**shairi | **D.**sayari |

***Kuanzia swali la 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Maana ya kujifunika gubigubi ni
A. kujifunika blanketi
B. kujifunika mpaka kiunoni
C. kujifunika kichwa tu
D. kujifunika mwili wote

17. Barua rasmi haina
A. anwani mbili
B. mintarafu
C. maamkizi
D. sahihi

18. Neno **mti** liko katika ngeli gani
A. KI - VI B. U - I
C. A - WA D. I - ZI

19. ***Andika kwa tarakimu***
Mia mbili na sita elfu, mia sita sitini na tatu
A. 206,663 B. 2006663
C. 206163 D. 2006163

20. Shairi la mishororo mitatu katika kila ubeti huitwa
A. Tarbia B. Tathlitha
C. Takhimisa D. Tathmina

21. Miongoni mwa sentensi zifuatazo ni ipi inaonyesha **'ki'** ya masharti
A. kitabu anachosoma ni kizuri
B. ukiwa umempata
C. ukija nitakulipa pesa zako
D. kiu kimemfanya anywe maji

22. Mbuzi ni aina ya mnyama, mbuzi pia ni
A. kifaa cha kuvunjia nazi
B. kifaa cha kukunia nazi
C. kifaa cha kunywea nazi
D. kifaa cha kubebea nazi

23. Maana ya **piga mbizi** ni
A. kuogelea
B. piga bila huruma
C. enda mbio
D. oga mwili

24. **Kamilisha methali hii**
Mgaaga na upwa hali wali
A. chache B. mingi
C. tamu D. mkavu

25. Tambua umbo hili




A. mstari mfuo
B. mstari sambamba
C. mstari wima
D. mstari sulubu

26. Ni ipi si kisawe cha jamaa
A. familia B. uzao
C. ukoo D. sahibu

27. Dadake mama yangu nitamwitaje?
A. Shangazi B. Halati
C. Binamu D. Mkoi

28. Ni ipi maana ya alama hii



A. kuna mzunguko mbele
B. mifugo hupita hapa
C. barabara telezi mbele
D. hatari

29. Akisami $^1/_3$ ni
A. Thuluthi B. Thumni
C. Humusi D. Sudusi

30. Kipeto ni cha barua kama vile thurea ni ya
A. wezi B. wanafunzi
C. wachawi D. nyota

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 - 40.***

Ilikuwa siku ya Jumatatu niliporauka asubuhi na mapema. Bwana shamsi alikuwa tayari ameshayeyusha umande wa alfajiri. Bila kusita nilirusha blanketi langu pembeni mwa kitanda na likaning'inia hapo kama popo topeni. Nilipiga magoti na kupiga bisimilahi kwa Dayani, waama mwomba Mola si mtovu.

Kabla ya sekunde kuunda dakika, nilisikia sauti dhoofu ikibisha mlangoni. Moyo ulinidunda dududu huku nikijiuliza kimoyomoyo mgeni huyo wa asubuhi alitoka wapi? Nilipomaliza kupiga dua nilisogea mlangoni ili kuisikiliza sauti ile kwa makini. Do! Nilisikia sauti iliyokuwa nyonge sana. Kwa umbali ilisikika kama sauti ya mtoto mchanga au ya mtu aliyekula chumvi nyingi.

Nilijawa na wasiwasi kwani kibanda changu hakikuwa na nafasi hata ya mgeni huyo kusimama. Kilinitosha mimi peke yangu. Sauti ilipoendelea kubisha, nilipiga moyo konde na kuamua kuufungua mlango. Mbele yangu alisimama bikizee. Baada ya kutazamana kwa muda wa kelbu kuukalia mkia wake huku nikijaribu kuifahamu sura yake, yule bikizee aliniomba mahali pa kupumzika na angalau chakula kidogo cha kutia kinywani. Niliamua kumpa kiporo changu cha pure, alikila kwa furaha na punde tu alipokimaliza alienda zake huku akisema kuwa Jalali anijalie

**31.** Kulingana na habari hii mwandishi

A. Alikuwa mkarimu

B. Alikuwa mchoyo

C. Alikuwa mjanja

D. Alikuwa mtundu

**32.** Bwana shamsi alikuwa tayari ameyeyusha umande wa alfajiri, huu ni wakati gani?

A. Alasiri B. Magharibi

C. Dhuha D. Macheo

**33.** Kupiga bismilahi ni?

A. Kuomba kabla ya majibu

B. Kufuturu

C. kudai baraka za Mungu

D. Kupiga dua

**34.** Lipi kati ya maneno haya si jina la mwenyezi Mungu?

A. Dayani B. Mahaluku

C. Rabana D. Rahimu

**35.** Sauti dhoofu aliyoisikia mwandishi

A. ilimfurahisha

B. ilimtia kiwewe

C. haikuwa ya yeyote

D. ilikuwa ya watoto

**36.** Mgeni huyo wa mwandishi alikuwa pale kwa kuwa

A. Alikuwa ni zawadi

B. Alikuwa ametumwa

C. Alihitaji usaidizi

D. Alikuwa mamaye mwandishi

**37.** Mwandishi wa makala haya alifanya nini kabla ya kwenda mlangoni?

A. Alikoga mwanzo

B. Alipiga dua

C. Alistaftahi

D. Alishtaki njaa

**38.** Sauti ilipozidi kubisha mlangoni mwandishi

A. Aliogopa na kujificha

C. Hakushughulika

C. Aliingiwa na hofu

D. Alipiga moyo konde

**39.** Chumba cha mwandishi kilikuwa cha aina gani?

A. Cha kifahari

B. Nyumba ya msonge

C. Kilikuwa kibanda

D. Ilikuwa kasri

**40.** Ni methali gani inayoweza kuelezea hali ya bikizee baada ya kupewa kiporo?

A. Penye nia pana njia

B. mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe

C. akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

D. simba mwenda pole ndiye mla nyama

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Siku moja mwanamke mmoja alikuwa akisafiri katika gari la abiria wakati wa usiku. Kumbe hakuwa na pesa za kutosha za nauli. Basi yule anayetoza pesa alipofika kwa mwanamke huyo, alimwomba atoe nauli yake. Yule mwanamke akatoa pesa alizokuwa nazo, lakini yule utingo akasema kuwa hazikutosha. Mama yule alimwelezea bwana huyo hakuwa na zaidi, akamwomba amsemehe. Bwana huyo alikataa kabisa akasema kwamba itambidi huyo mama atoke katika gari. Wasafiri wengine waliona uchungu sana hata mmoja wao akajitolea kumtolea yule bibi nauli, lakini utingo akasema hatakubali pesa za mtu mwingine yeyote, kwani yule mama alikuwa anazo pesa, ila alitaka kufanya **mzaha tu**. Mama alizidi kulia hata akatokwa na machozi naye yule mtu aliyejitolea, alisema hakuwa akifanya **mzaha** mama alitoka huku analia.

Alipoteremka tu akanaswa na kushambuliwa na simba. Kwa bahati, palitokea gari la polisi. Walilofukuza lile gari la abiria mpaka wakalishika. Walipoulizwa juu ya kisa hicho yule utingo alitaka kukana, lakini abiria wote walisema kwamba huyo mwanamke alikuwa katika basi hilo. Hapo basi yule utingo akashikwa na kupelekwa mahakamani. Akashtakiwa na kufungwa miaka kumi pamoja na viboko ishirini.

---

**41.** Mwanamke alikuwa akisafiri wakati wa

A. mchana B. asubuhi
C. usiku D. jioni

**42.** Mwanamke hakuwa na_______ya kutosha.

A. chakula B. nauli
C. nguo D. wasafiri

**43.** Neno **nauli** linamaanisha

A. pesa B. chakula
C. nguo D. wasafiri

**44.** Watu wanaosafiri kwa gari huitwa

A. abiria B. utingo
C. watalii D. msafara

**45.** Mtu anayeitisha pesa kwenye gari ni

A. mtalii B. utingo
C. sonara D. mfinyanzi

**46.** Mwanamke alitolewa nje ya gari wapi?

A. Kituoni B. Nyumbani
C. Mwituni D. Njiani

**47.** Ni mnyama yupi aliyemshambulia yule mwanamke?

A. Mbwa B. Fisi
C. Chui D. Simba

**48.** Neno ***'mzaha'*** limepigwa mstari linamaanisha

A. kumchezea mtu
B. kumtembelea mtu
C. kumwibia mtu
D. kuliwa

**49.** Utingo alishikwa na kupelekwa

A. mahakamani B. Jela
C. shuleni D. kanisani

**50.** Utingo alifungwa miaka mingapi

A. kumi B. sita
C. tano D. nne